
Washington State
Department of Social
& Health Services
Transforming lives

# Dondoo kuhusu Ovataimu na Ukomo wa Wiki ya Kazi kwa Mlezi Binafsi

**Wiki ya kazi ni:**

- Jumapili saa 12:00 a.m. hadi Jumamosi saa 11:59 p.m.
- Wiki ya kazi inaweza kupitisha vipindi vya malipo.
- Wiki ya kazi inaweza kupitisha miezi.




**Hutachukuliwa hatua za kimkataba kwa kufanya kazi zaidi ya kikomo chako cha wiki ya kazi kwa:**

- Mafunzo ya lazima ya DSHS
- Muda wa Safari Ulioidhinishwa
- Muda wa Kiutawala
- Likizo Yenye Malipo (PTO)

**Jinsi gani naweza kuepuka kuchukuliwa hatua za mkataba?**

- Daima panga ratiba yako ya kazi mapema kabla ya kazi kuanza na iandike.
- Ikiwa mahitaji ya mteja yatabadilika na ukalazimika kufanyakazi kwa ratiba nyingine ambayo inaathiri kikomo chako cha kazi cha wiki, wasiliana na meneja wa kesi wa mteja haraka sana.
- Rekodi muda wako wa kazi kwenye waraka wa kazi baada ya kila siku unayofanya kazi, pia inaweza kusaidia kurekodi muda katika kalenda ya karatasi. Kagua mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba unabaki ndani ya kikomo chako cha kazi cha wiki.
- DSHS ina vyanzo vinavyopatikana ili kukusaidia wewe na mwajiri/mteja wako kujifunza zaidi kuhusu kudhibiti ratiba yako ili kubaki ndani ya kikomo chako cha kazi cha wiki. Vyanzo hivi vinapatikana katika www.dshs.wa.gov/altsa/IPOT.

**Je, ni muda gani hatua za kimkataba zitabaki kwenye faili langu la mkataba?**

- Kila hatua ya kimkataba itandelea kubakia katika faili lako kwa miezi 12 kuanzia tarehe iliyopo juu ya notisi ya hatua ya kimkataba. Baada ya miezi 12, hatua hio ya kimkataba hufungwa.

**Mwezi uliotambuliwa katika mchakato wa uchukuaji wa hatua za kimkataba au barua hii ni mwezi wa malipo:**

- Kama barua inasema "kwa saa zilizolipwa katika mwenzi Apili," saa zilizofanyiwa kazi zinaweza kuhusisha saa zilizofanyiwa kazi mwezi wa nyuma yake (Machi).
- Wasiliana na msimamizi wa mteja wako kama una maswali kuhusu mwezi uliotuma madai zaidi.